TANGAZO LA SERIKALI NA. 747 la tarehe 16/12/2022

SHERIA YA MWENENDO WA MASHAURI YA JINAI
(SURA YA 20)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 204(1))*

AMRI YA UTEUZI WA WATAALAMU WA UCHUNGUZI WA ALAMA ZA VIDOLE YA MWAKA 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Uteuzi wa Wataalamu wa Uchunguzi wa Alama za Vidole ya Mwaka 2022.

Uteuzi wa wataalamu wa uchunguzi wa alama za vidole

2. Watu ambao majina yao yameorodheshwa katika Jedwali wanateuliwa kuwa wataalamu wa uchunguzi wa alama za vidole kwa madhumuni ya kutoa taarifa kama ushahidi katika shauri lolote la jinai chini ya Sheria na masuala mengine yanayohusiana.

Muda wa uteuzi

3.-(1)Muda wa uteuzi utakuwa ni miaka mitano kutoka tarehe ya kuanza kutumika kwa Amri hii.

(2) Bila kujali ujumla wa aya hii, mtu aliyeteuliwa chini ya Amri hii anaweza kufanya kazi kwa kipindi chini ya miaka mitano endapo ajira ya mtu huyo itafikia tamati au uteuzi wa mtu huyo utatenguliwa au kusitishwa na Mkurugenzi wa Mashtaka.

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na. | Jina |
|---|---|
| 1. | Pf. 22490 A/INP Ida Joseph Chaula |
| 2. | WP 3977 SGT Hamida |
| 3. | WP 4276 SGT Edina |
| 4. | G. 763 CPL Hashimu |
| 5. | G. 4302 CPL Charles |
| 6. | G. 8770 CPL Saimon |

Dodoma,
28 Oktoba, 2022

SYLVESTER ANTHONY MWAKITALU
*Mkurugenzi wa Mashtaka*